



NISHATI

HABARI ZA
NISHATI

News Bulletin

www.nishati.go.tz [Wizara ya Nishati](#) [wizara_ya_nishati_tanzania](#) [@Nishati2017](#) [Wizara ya Nishati](#)

Toleo Namba 42

Septemba 1 - 30, 2022

SEKTA YA NISHATI ITAENDELEA KUIMARISHWA ILI KUVUTIA WAWAKEZAJI ZAIDI - WAZIRI MKUU

>>> HABARI UK. 3



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan (kushoto) akipata maelezo kutoka kwa mmiliki wa Kiwanda cha Mbao cha TANWAT ambacho pia kinazalisha umeme, wakati wa ziara yake mkoani Njombe, Agosti 10, 2022. Wa pili Kulia ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato.



LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA
MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma

Energy Congress
2022 | Dar Es Salaam, Tanzania

Tanzania
Energy Congre
3 - 4 August 2022 | Dar Es Salaam, Ta



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Mhandisi Felchesmi Mramba
Katibu Mkuu

Makamu Mwenyekiti
Kheri Mahimbali

Mhariri
Dorina G. Makaya

Waandishi
Teresia Mhagama
Zuena Msuya
Hafsa Omar
Timotheo Mathayo

Msanifu Kurasa
Lucas Gordon

Wasiliana nasi kwa simu
namba +255-26-2322018
Nukushi: +255-26-2320148
au

Fika Ofisi ya Mawasiliano
Mitumba Dodoma,
S.L.P 2494, Dodoma



 www.nishati.go.tz

 [Wizara ya Nishati](#)

 [@Nishati2017](#)

 [wizara_ya_nishati_tanzania](#)

 [Wizara ya Nishati](#)

Sekta ya Nishati itaendelea kuimarishwa ili kuvutia wawekezaji zaidi - Waziri Mkuu

Na Zuena Msuya, DSM

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa, amesema kuwa Serikali itaendelea kusimamia kikamilifu na kuimarisha zaidi Sekta ya Nishati nchini ili kuvutia wawekezaji zaidi na kuondoa changamoto mbalimbali zinazojitokeza kwenye sekta.

Waziri Mkuu Majaliwa, alisema hayo wakati akifungua Kongamano la Nne la Nishati katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam, Agosti 3, 2022.

Alisema azma ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan,



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa (wa pili kulia waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake baada ya kufungua Kongamano la Nne la Nishati lililofanyika Jijini Dar es Salaam, Agosti 3, 2022, kulia kwake ni mwenyeji wa Kongamano hilo Waziri wa Nishati January Makamba.

ni kuweka mazingira wezeshi na rafiki kwa wawekezaji nchini ikiwemo kuwahakikishia utulivu na amani katika

kutekeleza majukumu yao kama sera ya nchi inavyoelekeza ili kuvutia wawekezaji wengi zaidi.

“Kongamano hili ni

muhimu sana kwa nchi yetu, litafungua fursa za uwekezaji nchini kutokana na kujumuisha makampuni mbalimbali



Waziri wa Nishati, January Makamba akizungumza na washiriki wa Kongamano la Nne la Nishati lililofanyika jijini Dar es Salaam, Agosti 3, 2022.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa (kulia) na Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (kushoto) wakizungumza jambo wakati wa Kongamano la Nne la Nishati lililofanyika Jijini Dar es Salaam, Agosti 3, 2022.

Sekta ya Nishati itaendelea kuimarishwa ili kuvutia wawekezaji zaidi - Waziri Mkuu

makubwa ya kimataifa katika sekta ya nishati, tuna wageni ambao ni wadau katika sekta ya nishati, hivyo litafungua fursa zilizopo kwenye Sekta ya nishati ikiwemo maji, mkaa ya mawe, gesi na umeme wa Jua," alisisitiza Majaliwa.

Alisema kuwa, utekelezaji wa miradi mbalimbali katika sekta ya nishati ikiwemo ya mafuta na gesi itasaidia kwa kiasi kikubwa katika kukuza uchumi wa nchi kutokana na mapato yatakayokuwa yanakusanywa kutoka kwenye miradi hiyo

Waziri Mkuu Majaliwa aliwataka washiriki wa kongamano hilo kujadili fursa zilizopo nchini, wajibu wao, nafasi yao ya kuwezekana nchini, pamoja na changamoto mbalimbali zinazoikabili

sekta hiyo ili serikali izifahamu na kuzifanyia kazi.

Kwa upande wake, Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba alisema Tanzania ina Rais ambaye ana matamano ya kuifanya sekta ya nishati kuwa chanzo cha ukuaji wa uchumi nchini.

Alisisitiza kuwa, Tanzania itaendelea kushirikiana na washirika wa kimataifa katika kukuza ushirikishwaji na uwezeshaji wa makundi mbalimbali kiuchumi katika sekta hiyo.

"Lengo la Serikali ni kutumia fursa za sekta yetu ya nishati ili kuboresha sekta nyingine ikiwemo viwanda, nina imani kwamba kongamano hili litawawezesha washiriki kubadilishana uzoefu, mawazo, ujuzi, maarifa,



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (kushoto), Kamishna wa Mafuta na Gesi Wizara ya Nishati, Michael Mjinja (wa Pili kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dkt. James Mataragio (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme (TANESCO), Maharage Chande (wa pili kulia) wakimsikiliza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa wakati akifungua Kongamano la Nne la Nishati lililofanyika jijini Dar es Salaam, Agosti 3, 2022.

ambayo ni muhimu katika kusimamia rasilimali nishati kwa njia sahihi na endelevu kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho," alisema Makamba.

Aliongeza kuwa, Serikali itaendelea kuhakikisha inaweka

kanuni na taratibu zinazofaa ili kuwezesha ushirikishwaji wa wafanyabiashara wa ndani kunufaika na mnyororo wa thamani katika sekta ya nishati.

Awali, Mkurugenzi wa Ocean Business Partners ambao ndio waandaaji



Viongozi na Maafisa wa Wizara ya Nishati wakiwa katika Banda la Wizara ya Nishati, wakati wa Kongamano la Nne la Nishati lililofanyika Jijini Dar es Salaam, Agosti 3, 2022.

Sekta ya Nishati itaendelea kuimarishwa ili kuvutia wawekezaji zaidi - Waziri Mkuu

wa kongamano hilo, Balozi Abdulsamad Abdulrahim alisema kongamano hilo litawawezesha wadau kutambua fursa za uwekezaji katika sekta ya nishati nchini

Alisema nchi 89, Watu zaidi ya 1000, Makampuni pamoja na wadau mbalimbali wa sekta ya nishati Duniani

wameshiriki katika Kongamano hilo la siku mbili.

Kongamano hilo lilihudhuriwa na Viongozi mbalimbali wa Wizara ya Nishati akiwemo Naibu Katibu Mkuu, Kheri Mahimbali, Wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara, pamoja na Maafisa kutoka Wizara na Taasisi hizo.



Mkurugenzi wa Idara ya Sera na Mipango wa Wizara ya Nishati, Petro Lyatuu (kushoto) na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), Charles Sangweni (kulia) wakimsikiliza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa wakati akifungua Kongamano la Nne la Nishati lililofanyika Jijini Dar es Salaam, Agosti 3, 2022.



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dkt. James Mataragio (katikati) akiwa katika banda la shirika hilo pamoja na maafisa wake wakati Kongamano la Nne la Nishati lililofanyika jijini Dar es Salaam, Agosti 3, 2022.



Kamishna Msaidizi wa Mafuta na Gesi wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Joyce Kisamo (kushoto) akimueleza jambo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alipotembelea banda la Wizara ya Nishati, wakati wa Kongamano la Nne la Nishati jijini Dar es Salaam, Agosti 3, 2022.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhhibiti huduma za Nishati na Maji (EWURA), Mhandisi Modestus Lumato (wa Pili kushoto) pamoja na maafisa wake wakiwa katika banda la Taasisi hiyo wakati wa Kongamano la Nne la Nishati jijini Dar es Salaam, Agosti 3, 2022.



Menyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dunstan Kitandula (kushoto) na Wajumbe wengine wa Kamati hiyo wakimsikiliza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa wakati akifungua Kongamano la Nne la Nishati lililofanyika Jijini Dar es Salaam, Agosti 3, 2022.

Milango iko wazi kuwekeza Sekta ya Nishati Zanzibar



Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah akizungumza wakati akifunga Kongamano la Nne la Nishati lililofanyika jijini Dar es salaam kwa siku mbili, Agosti 3 na 4, 2022.

Alisema kuwa, Serikali iko tayari kwa mazungumzo ya uwekezaji kwa kampuni ya aina yeyote ambayo iko tayari kuwekeza Zanzibar katika sekta ya nishati hasa mafuta na gesi kwa maslahi pande zote mbili ambazo ni Serikali na wananchi wake pamoja na muwekezaji husika.

Aliongeza kuwa, kwa sasa Zanzibar imepiga hatua kubwa katika sekta ya Mafuta na Gesi hivyo kampuni za uwekezaji zinakaribishwa ili kutekeleza miradi ambayo imebainika.

“Kongamano hili kubwa limefungua milango na kuongeza fursa zaidi za uwekezaji

Na Zuena Msuya DSM,

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imesema milango ya uwekezaji iko wazi kwa Wawekezaji, kuwekeza katika Sekta ya Nishati, hasa Mafuta na Gesi.

Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah alisema hayo wakati akifunga Kongamano la Nne la Kimataifa la Nishati lililofanyika jijini Dar es Salaam kwa siku mbili, Agosti 3 na 4, 2022.



Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Kamati ya Maandalizi ya Kongamano la Nne la Nishati lililofanyika jijini Dar es salaam kwa siku mbili, Agosti 3 na 4, 2022. Watatu waliokaa ni Waziri wa Nishati, January Makamba, na aliyesimama nyuma ya Makamu wa Pili wa Rais, ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali.

Milango iko wazi kuwekeza Sekta ya Nishati Zanzibar



Waziri wa Nishati, January Makamba (wa pili kulia) akizungumza wakati wa hafla ya utiaji saini makubaliano ya kuendeleza Miradi ya Nishati Jadidifu na Kampuni ya Masdar inayomilikiwa na Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu (U.A.E), Agosti 4, 2022, jijini Dar es salaam.

kwa nchi yetu, kwani wawekezaji walioshiriki katika kongamano hili wamefahamishwa juu ya fursa zilizopo kwa

upande wa Tanzania Bara na pia Zanzibar, hivyo waje tuzungumze katika masuala ya uchimbaji wa mafuta au ufuatiliaji

wa miradi mingine kwa maslahi ya pande zote mbili," alisisitiza Makamu wa Pili wa Rais Pia, aliipongeza

Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na wadau wengine katika kuandaa na kufanikisha kongamano hilo kubwa lililowakutanisha kwa pamoja wadau mbalimbali wa sekta ya nishati, ikiwepo makampuni makubwa zaidi ya 80.

Aidha alisema kuwa muitikio mkubwa wa washiriki katika kongamano hilo kutoka maeneo mbalimbali duniani, ni matokeo ya ziara za Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Mwinyi kutembelea nchi na makampuni makubwa mbalimbali duniani na kufanya nayo mazungumzo ya kutangaza fursa zilizopo nchini.

Kando ya Kongamano hilo, Wizara ya Nishati kupitia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)



Mhandisi Mkuu wa Mafuta na Gesi, Wizara ya Nishati, Mhandisi Joyce Kisamo (kushoto) akiwasilisha mada wakati wa Kongamano la Nne la Nishati lililofanyika jijini Dar es salaam kwa siku mbili, Agosti 3 na 4, 2022.



Kamishna wa Msaidizi wa Umeme Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga (wa pili kulia) akiwasilisha mada wakati wa Kongamano la Nne la Nishati lililofanyika jijini Dar es salaam kwa siku mbili, Agosti 3 na 4, 2022.

Milango iko wazi kuwekeza Sekta ya Nishati Zanzibar



Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizara ya Nishati, Petro Lyatuu, (kushoto) Katibu wa Naibu Waziri wa Nishati, Ngeleja Mgejwa (katikati) na Mjiolojia Mwandamizi kutoka Wizara ya Nishati Jacob Mayalla (kulia) wakimsikiliza Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah wakati akifunga Kongamano la Nne la Nishati lililofanyika jijini Dar es salaam kwa siku mbili, Agosti 3 na 4, 2022.

lilisaini makubaliano ya kuendeleza miradi

ya nishati jadidifu na Kampuni ya Masdar

inayomilikiwa na Serikali ya Umoja wa Falme za

Kiarabu (U.A.E).

Akizungumza wakati wa hafla ya utiaji saini, Waziri wa Nishati January Makamba, alisema kuwa makubaliano hayo ni matunda ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoifanya mapema mwaka huu katika nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu (U.A.E).

Alisema utekelezaji wa mkataba huo utasaidia kuongeza uzalishaji wa umeme kutoka vyanzo mbalimbali nchini.

Kwa upande wake Mkuu wa Uendelezaji wa Biashara na Uwekezaji wa Masdar, Abdullah Zayed alisema kuwa miradi iliyopo katika makubaliano hayo, uendelezaji wake unategemea kufikia Megawati 5000 kufikia mwaka 2025.



Mhandisi Mkuu wa Mafuta na Gesi, Joyce Kisamo (katikati) na Mhandisi Anita Ringia (kulia) wakimsikiliza Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah wakati akifunga Kongamano la Nne la Nishati, lililofanyika jijini Dar es Salaam kwa siku mbili, Agosti 3 na 4, 2022.



Mhandisi Rabia Issa kutoka Wizara ya Nishati, (katikati) akitoa maelezo kwa mmoja wa wananchi aliyetembelea banda la Wizara ya Nishati wakati Kongamano la Nne la Nishati lililofanyika jijini Dar es Salaam kwa siku mbili, Agosti 3 na 4, 2022. Anayeshuhudia ni Kamishna Msaidizi wa Gesi, Mohammed Fakihi (kulia).

WAZIRI MAKAMBA MWENYEKITI MPYA MRADI WA UMEME WA RUSUMO

Na Dorina Makaya - Rusumo, Kagera.

Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba, tarehe 20 Agosti, 2022, amekabidhiwa Uwenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa Mradi wa Umeme wa Rusumo utakaozalisha umeme kwa kutumia maji unaoshirikisha nchi tatu za Burundi, Rwanda na Tanzania.

Waziri Makamba amekabidhiwa jukumu hilo wakati wa Mkutano wa 14 wa Baraza la Mawaziri wa Mradi wa Umeme wa Rusumo na Waziri wa Miundombinu wa Rwanda Mhe. Mha. Dr. Ernest Nsabimana katika eneo la Mradi Rusumo,

Wilayani Ngara, Mkoani Kagera.

Mradi huo utazalisha Megawati themanini (80MW) ambapo kila nchi itapata 27MW.

Akizungumzia kuhusu jukumu jipya la Uwenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa Burundi, Rwanda na Tanzania katika Mradi wa Umeme wa Rusumo, Waziri Makamba amesema, Mradi wa Rusumo una miundo yake ya Uendeshaji ambapo kuna Baraza la Mawaziri, Bodi ya Kampuni na kamati ya Uendeshaji (Steering Committee) ambapo kila chombo kina kazi yake katika Mradi huo.

Alisema, kazi ya Baraza la Mawaziri, ni kutoa miongozo ya ki-sera kufuatilia, kusimamia,



Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba akizungumza na Waandishi wa Habari (hawamo pichani) wakati wa Mkutano wa 14 wa Baraza la Mawaziri wa Mradi wa Umeme wa Rusumo uliofanyika katika eneo la Mradi Rusumo, wilayani Ngara, mkoani Kagera. Tarehe 20 Agosti, 2022. Kushoto kwa Waziri Makamba ni Waziri wa Miundombinu wa Rwanda, Mhe. Mha. Dr. Ernest Nsabimana na kulia ni Waziri wa Maji Safi, Nishati na Madini wa Burundi, Mhe. Mha. Ibrahim Uwizeye.

kusukuma, na kuwezesha utekelezaji wa Mradi.

Waziri Makamba alieleza kuwa, Baraza hilo hukaa mara moja kwa mwaka na huomba taarifa ya Maendeleo ya Mradi

na kuelekeza kuharakisha utekelezaji wa Mradi

pamoja na kutoa maelekezo mahususi kwa ajili ya ufanisi wa Mradi na vyombo vyote vinaripoti kwenye Baraza



Mawaziri wa Burundi, Rwanda na Tanzania, wakipata maelezo ya maendeleo ya Mradi walipotembelea Mradi wa Umeme wa Rusumo tarehe 20 Agosti, 2022.

WAZIRI MAKAMBA MWENYEKITI MPYA MRADI WA UMEME WA RUSUMO

la Mawaziri.

Alieleza, Baraza hilo ni chombo muhimu katika uendeshaji wa Mradi huo na kasi ambayo imepatikana hivi sasa katika utekelezaji wa Mradi, kwa sehemu kubwa imetokana na Uongozi wa Baraza hilo la Mawaziri ambalo linatoa mchango mkubwa sana katika utekelezaji wa

Mradi.

Waziri Makamba alifanua kuwa, nchi hizo hupokezana Uwenyekiti ambapo kabla ya Rwanda nchi Mwenyekiti wa Baraza hilo ilikuwa ni Burundi, na sasa ni Tanzania.

Alieleza kuwa, jukumu lake la Uwenyekiti katika Baraza hilo la Mawaziri, litakuwa ni kuongoza

vikao na kuitisha vikao na kuwa na Mawasiliano ya moja kwa moja na Bodi kuhusu mambo ya kiutendaji ya kila siku yanayohitaji miongozo ya Mawaziri kabla, wakati na baada ya vikao pale inapohitajika.

Akizungumzia kuhusu Mradi wa Umeme wa Rusumo, Waziri Makamba alisema Mradi huo una

umuhimu mkubwa sana kwa maendeleo ya nchi zote tatu za Burundi Rwanda na Tanzania.

Aliueleza Mradi huo kuwa, ni ndoto ya viongozi waasisi wa nchi zote tatu kwa muda mrefu tangu miaka ya sitini ambapo, hatimaye ndoto hiyo inakaribia kukamilika.

Waziri Makamba



Mawaziri wa Burundi, Rwanda na Tanzania, wakipata maelezo ya maendeleo ya Mradi walipotembelea Mradi wa Umeme wa Rusumo tarehe 20 Agosti, 2022.



Picha za maeneo mbalimbali ya Mradi pamoja na mitambo itakayotumika kuzalisha umeme kama inavyoonekana pichani.

WAZIRI MAKAMBA MWENYEKITI MPYA MRADI WA UMEME WA RUSUMO

alisema, Mradi huo utaongeza umeme unaohitajika sana na wa bei nafuu katika nchi tatu hodhi za Mradi huo wa umeme wa Rusumo kutokana na mahitaji makubwa ya umeme na utakuwa ni chachu ya maendeleo kwa nchi hizo zinazoendelea.

Waziri huyo wa Nishati, aliongeza kuwa, Mradi huo unaashiria ushirikiano wa nchi hizo tatu zinazopakana na kuwa huo ni msingi wa maendeleo na unaashiria utashi wa nchi hizo tatu kutumia rasilimali asili zilizopo ikiwemo mito kuleta maendeleo ya watu wake.

Waziri Makamba alisema, kwa upande wa Tanzania, maeneo makubwa yanayozalisha umeme ni upande wa



Wajumbe wa Baraza la Mawaziri wa Mradi wa Umeme wa Rusumo wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji unaoshirikisha nchi tatu za Burundi, Rwanda na Tanzania wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kumalizika kwa mkutano wa 14 wa Baraza la Mawaziri wa Mradi wa Umeme wa Rusumo uliofanyika katika eneo la Mradi Rusumo, Wilayani Ngara, Mkoani Kagera, Tarehe 20 Agosti, 2022. Kutoka kulia ni Waziri wa Miundombinu wa Rwanda Mhe. Mha. Dr. Ernest Nsabimana, akifuatiwa na Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba na Waziri wa Maji Safi, Nishati na Madini wa Burundi, Mhe. Mha. Ibrahim Uwizeye.

kusini mashariki mwa Tanzania katika mikoa ya Iringa, Morogoro na Dar-es-salaam ambapo

kuna mitambo mingi ya kuzalisha umeme.

Alieleza kuwa, umbali wa kusafirisha umeme kutoka maeneo ya uzalishaji hadi upande wa Magharibi mwa nchi kuna umbali mkubwa, hivyo uwepo wa uzalishaji umeme katika eneo la Rusumo utaongeza upatikanaji wa umeme katika Gridi ya Taifa na maeneo yaliyopo karibu na eneo la Mradi yatapata umeme wa uhakika bila kuusafirisha kutoka umbali mrefu.

Waziri Makamba aliwaambia Watanzania kuwa, wategemee kunufaika na Mradi wa Umeme wa Rusumo ndani ya Kipindi cha miezi 6 kuanzia sasa na mradi huo unategemewa kukamilika mwezi Novemba mwaka huu ambapo Mtambo wa kwanza utaanza kujaribiwa kuwashwa na umeme unatarajiwa kuanza kupatikana katika robo ya kwanza ya mwaka 2023.



... kwa upande wa Tanzania, maeneo makubwa yanayozalisha umeme ni upande wa kusini mashariki mwa Tanzania katika mikoa ya Iringa, Morogoro na Dar es salaam ambapo kuna mitambo mingi ya kuzalisha umeme."

Mafuta hayajashuka bei katika soko la Dunia, Tanzania tumeshusha Bei- Byabato

**Na Zena Msuya,
Njombe**

Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato amesema kuwa Serikali kupitia Wizara ya Nishati, imekuwa ikitenga fedha maalum kila mwezi ili

kupunguza gharama za mafuta kwa watumiaji kutokana na bidhaa hiyo kuendelea kupanda bei katika soko la Dunia.

Byabato alisema hayo wakati akiwasalimia wananchi kwenye Mkutano wa hadhara uliofanyika katika Uwanja Sabasaba wakati wa

Ziara ya Rais, Mhe. Samia Suluhu Hassan, mkoani Njombe Agosti 10, 2022.

Wakili Byabato alifafanua kuwa, kutokana na kuendelea kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia, kwa sababu mbalimbali, Serikali imekuwa ikitenga shilingi

Bilioni 100 kila mwezi ili kuwapunguzia wananchi gharama za kununua mafuta hayo.

Aliweka wazi kuwa, fedha hiyo inayotengwa na Serikali imewezesha kupunguza shilingi 200 hadi 300 katika kila lita moja ya mafuta ya Petroli, na shilingi 400



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akiongea na Wananchi kwenye mkutano wa hadhara katika Uwanja vya Sabasaba, wakati wa ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan, mkoani Njombe, Agosti 10, 2022.

Mafuta hayajashuka bei katika soko la Dunia, Tanzania tumeshusha Bei- Byabato

kwa kila lita moja ya Mafuta ya Dizeli.

Katika ziara hiyo ya Rais, Naibu Waziri aliambatana na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali pamoja na Viongozi wa Taasisi zilizo chini ya wizara hiyo.

Akizungumzia masuala ya Nishati ya Umeme katika Mkoa huo wa Njombe, Byabato alisema Serikali imetenga fedha za kutosha kuweza kutatua changamoto ya Umeme mkoani humo ikiwa ni pamoja na kuongeza kasi ya kusambaza umeme



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, (katikati) akimsikiliza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, (hayupo pichani) alipotembelea Kiwanda cha mbao cha TANWAT ambacho pia kinazalisha umeme, wakati wa ziara ya Rais mkoani Njombe, Agosti 10, 2022.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan (katika) akizungumza na Wananchi kwenye mkutano wa hadhara katika uwanja wa Sabasaba wakati wa ziara yake Mkoani Njombe, Agosti 10, 2022.

katika Vijiji na Vitongoji.

Vilevile wakandarasi wanaendelea na kazi katika maeneo mbalimbali kuhakikisha miradi ya usambazaji wa umeme inatekelezeka wananchi kupata huduma.

Aidha alieleza kuwa, Serikali imetenga shilingi Bilioni 8 katika maandalizi ya kazi za awali za kutekeleza Mradi wa kufua umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Rumakali.

TANZANIA NA OMAN KUSHIRIKIANA KUKUZA SEKTA YA NISHATI

Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba amekutana na Balozi wa Oman nchini Tanzania Mhe. Saud Hilal Al Shidhani na kuzungumzia fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo katika sekta ya mafuta na gesi hususani katika miradi mikubwa inayoendelea kutekelezwa nchini.

Mazungumzo hayo yalifanyika katika ofisi ndogo ya Wizara ya Nishati jijini Dar es Salaam tarehe 16 Agosti, 2022 na yalijikita katika kuzungumzia makubaliano mbalimbali yaliyofikiwa wakati wa ziara ya Rais wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan nchini Oman Juni, 2022.

Kupitia Mazungumzo hayo Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC) litashirikiana

na Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Oman (OQ) kufanya biashara ya mafuta ya jumla (fuel supply), kujenga vituo vikubwa vya gesi za mitungi (LPG) na kushirikiana na Kampuni Tanzu ya TPDC (TANOIL) ili kufanya biashara ya rejareja ya mafuta.

Halikadhalika, wataalamu kutoka nchini Oman wataendelea kuja nchini Tanzania kuangalia miundombinu ya Bandari na kutazama maeneo ya kuwekeza kwenye miundombinu ya kupokea, kushusha, kuhifadhi na kutoa mafuta katika Bandari na Ghala za dhamana ya forodha pamoja na kubadilishana uzoefu na Tanzania.

Waziri wa Makamba wakati wa mazungumzo hayo alisema Tanzania inatafuta Washirika wa

kimkakati ambao watashirikiana na TPDC katika kutafuta mafuta na gesi katika vitalu vilivyopo ili kuchochea ukuaji wa viwanda na kuongeza ukuaji wa uchumi nchini hususan katika miradi ya kimkakati ukiwemo wa Mwalimu Julius Nyerere.

Akizungumza katika Mkutano huo Mhe. Balozi Saud Hilal Al Shidhani pamoja na kutoa salaam za Rais wa Oman alimshukuru Rais wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa utayari wake wa kushirikiana na Oman katika kuendeleza sekta ya nishati.

Aidha, alisema Oman ina ujuzi mkubwa katika masuala ya mafuta hivyo alimhakikishia Waziri Makamba kuwa watashirikiana vyema katika kukuza sekta hiyo nchini Tanzania.



Matukio mbalimbali wakati Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba alipokutana na Balozi wa Oman nchini Tanzania Mhe. Saud Hilal Al Shidhani na kuzungumzia fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo katika sekta ya mafuta na gesi.

Ujenzi ofisi ya Wizara ya Nishati washika kasi



Muonekano wa jengo la ofisi za Wizara ya Nishati, (upande wa nyuma wa jengo), linalojengwa katika Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma, Agosti 12, 2022.

Na Timotheo Mathayo, **Dodoma.**

Wizara ya Nishati inaendelea kwa kasi kutekeleza mradi wa Ujenzi wa Ofisi katika Mji wa Serikali wa Mtumba uliopo jijini la Dodoma ikiwa ni mkakati wa Serikali kusogeza huduma kwa wananchi.

Ujenzi wa Ofisi hiyo utakapokamilika

utasaidia kuwaleta pamoja Watumishi wa Wizara ya Nishati ili kuweza kutoa huduma kwa wananchi katika eneo moja, tofauti na ilivyo sasa.

Hayo yalibainishwa tarehe 12 Agosti, 2022 na Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu, Wizara ya Nishati, Bi. Ziana Mlawa ambapo alisema kuwa ujenzi wa jengo la ofisi yenye ghorofa tano umefikia asilimia

35 na Mkandarasi wa jengo hilo ni Shirika la Nyumba la Taifa (NHC). Aliongeza kuwa jengo linasimamiwa na mshauri mwelekezi, Chuo kikuu cha Ardhi kupitia kampuni tanzu ya ABECK.

Ujenzi wa jengo la ofisi za Wizara ya Nishati ulianza Novemba 29, 2021 kwa mujibu wa mkataba uliosainiwa kati ya NHC na Wizara ya Nishati ambapo mradi

huo utatekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili na unatarajiwa kukamika ifikapo mwaka 2023.

Msimamizi wa Jengo hilo, Bw. Alphonse Kilovele, kutoka Wizara ya Nishati alisema kuwa ujenzi wa nguzo, kuta, umwagaji zege kwenye msingi, sakafu pamoja na bimu hatua hizo zote zinatakiwa kukamilika ndani ya miezi kumi na mbili na hatua zote zimetatekelezwa kwa

Ujenzi ofisi ya Wizara ya Nishati washika kasi



Mkuu wa kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Bi. Dorina G. Makaya (wa kwanza kushoto), akikagua na kutazama maendeleo ya Ujenzi wa jengo la ofisi za Wizara ya Nishati, Agosti 12, 2022.



Muonekano wa jengo la ofisi za Wizara ya Nishati (upande wa mbele wa jengo), linalojengwa katika Mji wa Serikali Mtumba, Jijini Dodoma, Agosti 12, 2022.

zaidi ya asilimia 35 na zimebaki asilimia 15 kukamilika.

Kazi ya kuweka mfumo wa umeme, mifumo ya maji safi na maji taka, ujenzi wa uzio, usafi wa jengo pamoja na kazi nyingine ndogondogo ni sehemu ya asilimia hamsini iliyobaki ambazo zitatekelezwa ndani ya miezi 12 kwa mujibu wa mkataba.

Bw. Kilovele alisema mradi huo wa ujenzi unahusisha vibarua kati ya 92 hadi 105 kila siku, hii ni kulingana na mahitaji ya kazi zinazotakiwa kufanyika kwa mujibu wa ratiba ya kazi.



Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu kutoka Wizara ya Nishati Bi. Ziana Mlawa (wa pili kulia) akikagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la ofisi za Wizara ya Nishati, linalojengwa katika Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma, Agosti 2022.

BAJETI YA MATENGENEZO YA MIUNDOMBINU YA UMEME YAONGEZWA KUIMARISHA UPATIKANAJI UMEME



Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba, akizungumza na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakati Wizara ilipowasilisha kwa Kamati hiyo, utekelezaji wa maazimio ya Bunge kutokana na taarifa ya mwaka ya Kamati kwa kipindi cha mwezi Februari 2022.

Serikali imeongeza bajeti ya matengenezo ya miundombinu ya umeme kutoka shilingi bilioni 197.61 kwa mwaka 2021/2022 hadi shilingi bilioni 211.56 kwa mwaka 2022/2023 ili kuimarisha hali ya upatikanaji umeme nchini.

Hayo yameelezwa bungeni, jijini Dodoma wakati Wizara ya Nishati ikiongozwa na Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba ilipowasilisha kwa Kamati ya Kudumu

ya Bunge ya Nishati na Madini, utekelezaji wa maazimio ya Bunge kutokana na taarifa ya mwaka ya Kamati hiyo kwa kipindi cha mwezi Februari 2022.

Kamati hiyo imeelezwa kuwa, ongezeko hilo la bajeti limefanywa ili kuhakikisha matengenezo ya miundombinu yanafanyika kikamilifu na kwa wakati na hivyo kuimarisha hali ya upatikanaji umeme.

Pamoja na hilo,

Serikali imetenga shilingi Bilioni 500 kwa ajili ya mradi wa kuimarisha gridi ya Taifa ambao unalenga kuboresha hali ya umeme nchini ambapo pamoja na kazi nyingine, jumla ya kilometa 3,930 za njia ya usafirishaji umeme zitajengwa, jumla ya vituo vikubwa vya umeme 62 vitajengwa na kilometa 2,572 za njia za usambazaji umeme zitajengwa pia.

Kuhusu utekelezaji wa mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) Kamati hiyo imeelezwa kuwa, mradi huo ambao utekelezaji wake umefikia asilimia 67.18, unaendelea kutekelezwa kwa ufanisi



Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande, akizungumza wakati wa Kikao cha Wizara ya Nishati na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakati Wizara ilipowasilisha kwa Kamati hiyo utekelezaji wa maazimio ya Bunge kutokana na taarifa ya mwaka ya Kamati kwa kipindi cha mwezi Februari 2022.

BAJETI YA MATENGENEZO YA MIUNDOMBINU YA UMEME YAONGEZWA KUIMARISHA UPATIKANAJI UMEME



Watendaji mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati na Taasisi zilizo chini ya Wizara wakifuatilia Kikao cha Wizara ya Nishati na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakati Wizara ilipowasilisha kwa Kamati hiyo utekelezaji wa maazimio ya Bunge kutokana na taarifa ya mwaka ya Kamati kwa kipindi cha mwezi Februari 2022.

kwani kuna vitengo kutoka Wizara ya Nishati na TANESCO ambavyo vinasimamia mradi huo na pia kuna kamati ya Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali wanaosimamia mradi.

Aidha, ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji umeme wa kV 400 kutoka JNHPP hadi Chalinze ambapo kunajengwa pia kituo cha kupoza umeme, imefikia asiliamia 60 na inatarajiwa kukamilika mwezi Januari mwaka

2023 hali itakayowezesha umeme kutoka mradi huo kutokumbwa na changamoto ya usafirishaji na usambazaji.

Kuhusu suala la ujenzi wa maghala makubwa ambayo yatahifadhi mafuta zaidi ya mita za ujazo milioni 1.25 na kuiwezesha nchi kuagiza mafuta mengi zaidi wakati bei ya mafuta inaposhuka katika soko la dunia, Serikali imeeleza kuwa Shirika la Maendeleo ya Petrol

Tanzania (TPDC) kwa kushirikiana na kampuni yake ya TANOIL imeanza utekelezaji wa kujenga maghala makubwa ya kuhifadhi mafuta (tank farms) ambapo yatatumika pia kama hifadhi ya Taifa ya mafuta ya kimkakati.

Kikao hicho cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kilihudhuriwa pia na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, kheri Mahimbali, Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Edward Ishengoma, Kamishna wa Petroli na Gesi, Michael Mjinja, Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Petro Lyatuu na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati.



Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, wakiwa katika kikao na Wizara ya Nishati ilipowasilisha kwa Kamati hiyo utekelezaji wa maazimio ya Bunge kutokana na taarifa ya mwaka ya Kamati kwa kipindi cha mwezi Februari 2022.

Serikali kuendelea kuimarisha huduma za Umeme Vijijini



Mwenyekiti wa kamati ya kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mhe. Daniel Sillo Baran, akiongoza kikao, wakati wa kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Nishati Vijijini, kilichofanyika bungeni jijini Dodoma, Agosti 30, 2022.

mengine, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ilitaka kujua bei ya kuunganishia wateja wapya waliopo maeneo ya vijijini kutofautiana.

Byabato alisema kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Nishati imekwishaunda timu ya wataalam ambayo iko kazini ili kuona uhalisia na hatimaye kuja na bei inayoendana na mazingira ya wananchi waishio katika maeneo ya Vijijini.

Wajumbe wa kamati ya Bunge, waliipongeza Taasisi ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwa kazi nzuri inayotekelezwa na Wakala huo.

Kikao hicho, kilihudhuriwa na

Na. Godfrey Mwemezi

Serikali imeendelea na mikakati mbalimbali ili kuhakikisha inaendelea na utekeleza wa Miradi ya kusambaza umeme Vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Hayo, yamesemwa na Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Wakili Stephen Byabato wakati wa kikao cha kamati ya kudumu ya Bunge ya Bajeti kilichofanyika Bungeni Jijini dodoma, Agosti, 30, 2022.

Pamoja na mambo



Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Wakili Stephen Byabato akizungumza wakati wa kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge la Bajeti kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Nishati Vijijini, kilichofanyika bungeni jijini Dodoma, Agosti 30, 2022.

Serikali kuendelea kuimarisha huduma za Umeme Vijijini



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mha. Felchesmi Mramba, Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mha. Hassan Seif Saidu, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Renata Ndege na Wataalam mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati pamoja na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).




Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba (wa kwanza kulia), akiwa na Mkurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini, Mha. Hassan Seif Saidu (wa kwanza kushoto), wakiwa kwenye kikao cha kamati ya kudumu ya Bunge ya Bajeti kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Nishati Vijijini kilichofanyika jijini Dodoma, Agosti 30, 2022.



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, wakiwa kwenye kikao cha kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Nishati Vijijini, kilichofanyika katika Ukumbi wa Bunge, Jijini dodoma, Agosti 30, 2022.

JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI



Fika Ofisi ya Mawasiliano,
Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018
Nukushi +255-26-2320148

 www.nishati.go.tz

 [Wizara ya Nishati](https://www.facebook.com/Wizara.ya.Nishati)

 [@Nishati2017](https://twitter.com/Nishati2017)

 [wizara_ya_nishati_tanzania](https://www.instagram.com/wizara_ya_nishati_tanzania)

 [Wizara ya Nishati](https://www.youtube.com/Wizara.ya.Nishati)